


MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TANZANIA KIPINDI CHA JUNI - AGOSTI (JJA), 2021



Dondoo muhimu za hali ya hewa kipindi cha Juni-Agosti (JJA), 2021

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na hali ya hewa inayotarajiwa katika msimu wa Kipupwe kwa miezi ya Juni hadi Agosti (JJA), 2021; Ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa kawaida, kipindi cha miezi ya Juni hadi Agosti (JJA), huwa ni kipindi cha baridi na kipupwe kwa maeneo mengi ya nchi.

Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

a) Viwango vya joto

- Kwa ujumla katika kipindi cha JJA, 2021 hali ya joto la chini inatarajiwa kuwa ya kawaida katika maeneo mengi ya nchi.
- Hali ya joto la chini inatarajiwa kuwa ya juu kidogo ya kiwango cha kawaida katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki, ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Aidha katika maeneo ya kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi na mkoa wa Ruvuma hali ya joto la chini inatarajiwa kuwa chini kidogo ya joto la kawaida kama ilivyozeleka.
- Vipindi vya baridi kali zaidi vinatarajiwa kujitokeza mwezi Julai.
- Vipindi vya baridi kali vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini magharibi hususan nyakati za usiku na asubuhi.

b) Upepo

- Katika kipindi cha miezi ya Juni na Agosti, 2021 vipindi vya upepo mkali wa Kusi vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Zaidi ya hapo, katika msimu wa mwaka huu, vipindi vya upepo unaovuma kutoka kusini-mashariki na mashariki (Matlai) vinatarajiwa katika ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi na maeneo ya mwambao wa pwani hususan mwezi June, 2021. Hali hii inatarajiwa kuleta unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi na kusababisha vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya visiwa vya Unguja na Pemba, pamoja na ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara).

c) Athari

- Hali ya ukavu, upepo na ubaridi inaweza kusababisha athari kwa binadamu, wanyama na mazao.
- Jamii inashauriwa kuchukua hatua za tahadhari ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi mazuri ya maji na kujikinga ili kupunguza athari mbaya zinazoweza kusababishwa na hali ya hewa inayotarajiwa.

1.0 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha msimu wa kipupwe (mwezi Juni hadi Agosti), 2021, hali ya joto la bahari katika ukanda wa tropiki ya kati ya bahari ya Pasifiki (CEPO) inatarajiwa kuwa ya chini ya wastani. Aidha, hali ya kawaida ya joto la bahari inatarajiwa upande wa magharibi mwa bahari ya Hindi, wakati joto la bahari ya juu ya wastani linatarajiwa katika ukanda wa mashariki wa bahari ya Hindi. Hali kadhalika, joto la kawaida la bahari linatarajiwa mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola). Kwa ujumla, hali hii ya joto inayoonekana kwenye bahari zote inaashiria kuwepo kwa hali ya ukavu katika maeneo mengi ya nchi.

Hali ya joto la bahari katika eneo kubwa la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (kusini mashariki mwa kisiwa cha Madagascar) inatarajiwa kuwa juu kidogo ya wastani, wakati huohuo hali ya kawaida ya joto la bahari inatarajiwa pwani ya magharibi mwa Australia. Hali hii inatarajiwa kupunguza nguvu ya mgandamizo mkubwa wa hewa (Mascarine high pressure) pamoja na madhara yake katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo kupunguza uwepo wa vipindi vya upepo mkali na hali ya ubaridi kwenye maeneo mengi ya nchi.

2.0 MATARAJIO YA VIWANGO VYA JOTO KWA MIEZI YA JUNI HADI AGOSTI, 2021

Kwa ujumla katika kipindi cha JJA, 2021 hali ya joto la chini inatarajiwa kuwa ya kawaida kama ilivyozoeleka katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, hali ya joto la chini inatarajiwa kuwa ya juu kidogo ya kiwango cha kawaida katika maeneo ya ukanda wa Pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki, ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hali kadhalika, maeneo ya kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi na mkoa wa Ruvuma hali ya joto la chini inatarajiwa kuwa chini kidogo ya joto la kawaida kama ilivyozoeleka. Hata hivyo, vipindi vya baridi kali vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini magharibi hususan nyakati za usiku na asubuhi. Aidha, vipindi vya baridi kali vinatarajiwa kujitokeza katika mwezi wa Julai.

2.1 Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Shinyanga na Simiyu):
Kiwango cha joto la chini ("minimum temperature") kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi juu ya kawaida kati ya nyuzi joto 14 na 19 katika maeneo mengi.

2.2 Ukanda wa pwani ya kaskazini (Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Joto la chini linatarajiwa kuwa la kawaida hadi juu ya kawaida kama ilivyozoeleka katika maeneo mengi, kiwango hicho kinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 na 23. Hata hivyo, maeneno yenye miinuko hususan katika mikoa ya Tanga na Morogoro yanatarajiwa kuwa na kiwango cha nyuzi joto chini ya 18.

2.3 Kanda ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):

Katika msimu huu kwa ujumla kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi juu ya kawaida kati ya *nyuzi joto 10 na 17* katika maeneo mengi. Aidha, katika maeneo ya miinuko kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa chini ya *nyuzi joto 10*.

2.4 Kanda ya magharibi (Mikoa ya Tabora, Rukwa, Katavi na Kigoma):

Kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi juu ya kawaida kama ilivyozoeleka kati ya *nyuzi joto 13 na 19* katika maeneo mengi.

2.5 Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi chini ya kawaida, kati ya *nyuzi joto 10 na 17* katika maeneo mengi.

2.6 Ukanda wa pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):


Kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi juu ya kawaida kama ilivyozoeleka, kati ya *nyuzi joto 18 na 23* katika maeneo mengi.

2.7 Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):

Kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi chini ya kawaida kati ya *nyuzi joto 11 na 14* katika maeneo mengi.

2.8 Kanda ya nyanda za juu kusini-magharibi (Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe pamoja na maeneo ya kusini ya mkoa wa Morogoro):

Maeneo mengi yanatarajiwa kuwa na joto la chini la kawaida hadi chini ya kawaida, kati ya *nyuzi joto 6 na 14*. Aidha, kiwango cha joto la chini katika maeneo ya miinuko kinatarajiwa kuwa chini ya *nyuzi joto 6*.



Picha 1: Mwelekeo wa viwango vya joto la chini katika msimu wa JJA, 2021

Picha 2: Wastani wa muda mrefu wa viwango vya joto la chini kwa msimu wa Juni hadi Agosti.

3.0 MWENENDO WA UPEPO KWA KIPINDI CHA JUNI HADI AGOSTI (JJA), 2021

Kwa kawaida msimu wa kipupwe hutawaliwa na upepo wa *Kusi*. Kutokana na matarajio ya uimarikaji wa wastani wa mgandamizo mkubwa wa hewa kusini mwa Afrika vipindi vichache vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza. *Hata hivyo*, katika kipindi cha miezi ya Juni na Agosti, 2021 vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Zaidi ya hapo, katika msimu wa mwaka huu, vipindi vya upepo unaovuma kutoka kusini-mashariki na mashariki (Matlai) vinatarajiwa katika ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi na maeneo ya mwambao wa pwani hususan mwezi June, 2021. Hali hii inatarajiwa kuleta unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi na kusababisha vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya visiwa vya Unguja na Pemba, pamoja na ukanda wa Pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara). Aidha, katika ukanda wa Ziwa Victoria vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache.

4.0 ATHARI NA USHAURI

Hali ya baridi inayotarajiwa hususan maeneo yenye miinuko ya Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe), inaweza kuleta athari kwa binadamu, wanyama, samaki pamoja na ustawi wa mazao mashambani hususani mazao ya muda mrefu kama migomba yanaweza kupata magonjwa ya fangasi na kudhoofisha ustawi wake. Kutokana na hali ya joto katika bahari ya Hindi kuwa juu ya wastani, ongezeko la tija katika shughuli za uvuvi katika kipindi cha msimu huu linatarajiwa.

Hali ya ukavu na upepo inaweza kuongeza upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo na kuathiri upatikanaji wa maji kwa mazao, mifugo na matumizi mengine. Hivyo, Jamii inashauriwa

kuchukua hatua za tahadhari ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi mazuri ya maji na kujikinga ili kupunguza athari mbaya zinazoweza kusababishwa na hali ya hewa inayotarajiwa.

Mwelekeo wa hali ya hewa uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya hewa katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa.

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania: